

Pambazuko

Toleo Namba 062

Jumatatu Februari 19-25 2024

Atamani Afrika itawaliwe tena

- Adai viongozi wengi wabakhirifu, waongo
- Asema hakuna demokrasia, utawala bora

Uk. 6

TUNATAKA KATIBA MPYA TANZANIA



Wanaharakati wa haki za binadamu katika Jiji la Roma, Italia, wakibeba mabango kumhimiza Rais Samia Suluhu Hassan kuharakisha machakato wa kupatikana kwa katiba mpya kabla ya uchaguzi mkuu wa Tanzania, mwaka kesho.

Jicho la Tai

Uk. 5

'Sukari anasa, weka majivu kwa chai'

Walawiti, wabakaji kukatwa uume Uk 18

Tumechoka mateso ya CCM – Lissu... Uk 8



JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

Tahariri

Hili la umeme ni aibu kwa viongozi wetu

SIYO mara moja ama mbili, bali mara nyingi tu, viongozi wa serikali waliopo madarakani na hata waliopita, wamekuwa wakitoa kauli za ahadi zenye matumaini makubwa kutatua kero nyingi za Watanzania.

Kauli hizo zimekuwa zikitolewa na marais, mawaziri wakuu na mawaziri kuhusu kupungua ama kumalizika kwa baadhi ya kero zinaziokabili jamii.

Baadhi ya kero, ni kama zimeshinda serikali zote; tangu Tanzania ipate uhuru wake, Desemba 9, 1961, baada ya Uingereza kukoma kuitawala nchi hiyo ya Afrika Mashariki.

Kero zinazoonekana kushinda serikali zote za awamu sita, ni nyingi, lakini kubwa ni suala zima la kupatikana kwa nguvu za uhakika za kuzalisha na kusambaza nishati ya umeme.

Kila serikali; kuanzia awamu ya kwanza wakati wa uongozi wa Mwalimu Julius Nyerere, pamoja na kuwa na idadi ndogo ya watu, bado umeme ulikuwa tatizo, hasa kuanzia mwaka 1965. Matangazo yapo mengi kwenye vyombo vya habari kuthibiisha hili.

Baadaye akafuata rais wa awamu ya pili, Alhaj Ali Hassan Mwinyi, mambo yakawa yaleyale. Umeme ukawa shida kubwa. Tatizo likaendelea na akaondoka na kuliacha.

Akafuata, Rais Benjamin Mkapa katika awamu yake ya tatu. Akapambana kwa kutoa ahadi lukuki kwamba wakati wake kero ya umeme itaondoka. Hola! Akaondoka, baada ya miaka yake 10, na kuiacha.

Rais Jakaya Kikwete, akaingia

madarakani akiwa na kaulimbiu yake ya 'maisha bora kwa kila Mtanzania,' akaahidi kuifuta historia ya kero ya umeme, lakini akakwama! Akaondoka na kuacha kero palepale.

Baada ya miaka yake 10 ya uongozi, akaingia Rais John Magufuli. Huyu akiwa na kaulimbiu yake ya "hapa kazi tu," akafurukuta. Huduma ya umeme ikaonekana kuimarika. Watanzania wakafurahia na kupongeza kwamba sasa kero ya umeme imepata mwamba wa kuitatua.

Katika kipindi chake, kukatika kwa umeme ikawa nadra mno, na Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (Tanesco), likaimarisha utaratibu wa kutoa taarifa mapema pale kunapotokea ulazima wa kukata umeme kwa eneo fulani.

Hata hivyo, baada ya kufariki dunia kwa Rais Magufuli, akiwa amehudumu kwenye nafasi ya urais kwa miaka mitano na ushei, akaingia Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye baada ya muda mfupi wa uongozi wake, Watanzania wakaanza kuonja shubiri tena ya kero ya umeme.

Wengi wakajiuliza, kulikoni kero ya umeme kurejea na kutesa wananchi? Jibu likawa jepesi tu, kwamba Rais Magufuli alikuwa akigomea ushauri wa wataalamu wa nishati kufanya marekebisho na maboresho ya mitambo, ambayo baadaye ingeweza kuiweka nchi gizani. Kwamba lilikuwa suala la muda tu.

Sasa basi, sisi Pambazuko tunauliza, shida ya kukosekana nishati hiyo ni nini hasa? Au kuna hujuma?

BURIANI EDWARD LOWASSA...



Rais Samia Suluhu Hassan akisaini kitabu cha maombolezo nyumbani kwa waziri mkuu mstaafu, hayati Edward Ngoyai Lowassa, Monduli, Arusha. Lowassa aliyefariki Februari 10, 2024, alizikwa jana huko Monduli. Rais Samia aliongoza shughuli za mazishi hayo ya kitaifa (Picha na Ikulu).

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko.tza@gmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

NUKUU



Hakuna vazi lolote duniani linaloitwa la taifa, lililoundiwa tume. Hakuna! Kuwafanya Watanzania watumie muda wao kusaka vazi la taifa ni wild-goose chase (wehu) na mbinu ya kuwafanya wasahau mambo muhimu yaliyowashinda watawala. Tusipotezeane muda wetu - Jenerali Ulimwengu, Februari, 2024.

Tangazo

Tuchangie

Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako na wale wengine tuliowaomba kuchagia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**

Mhariri Mkuu,
Oktoba, 2023

Changia Pambazuko liendelee

WAJUMBE wa Bodi ya Uhariri, Mhariri Mkuu, wahariri, waandishi na watendaji wote wa gazeti la Pambazuko wameendelea kufuraha kusambaza habari, makala, safu, maoni, picha kwa miezi 15 bure kwa wasomaji wake.

Katika kipindi chote hicho cha kusambaza habari bila malipo, watendaji wa Pambazuko wamekuwa wakituma fedha, muda, ujuzi na rasilimali zingine kuhakikisha kila Jumatatu, gazeti hili linawafikia zaidi ya watu 500,000 duniani kote, bila malipo.

Ikumbukwe kwamba wazungumzaji wa lugha adhimu ya Kiwahili duniani kote; wanalitumia gazeti hili siyo kwa kupata habari tu, bali hata kusambaza kwa wengine kujifunza lugha hiyo inayokuwa zaidi kwa sasa.

Katika kipindi cha uhai wa gazeti hili - miezi 15, mengi mazuri yamepatikana, mbali na kukua Kiwahili, kuhabarisha, kupaza maoni ya watu, lakini pia Pambazuko limeviza kusukuma watoto uamuzi, hasa serikali kuchukua hatua kwenye baadhi ya mambo ambayo yameweka wazi kwa umma. Gazeti hili limesaidia kuepusha majanga, kuponya majaraha na zaidi sana, kuunganisha jamii na kuchochea umoja na kumarisha amani.

Pamoja na mafanikio hayo makubwa - na bado yanaendelea, uongozi wa Pambazuko umepokea mawazo kwamba gazeti hili linazoe kusuzwa, lakini hasi kubaliana na mawazo ya idadi kubwa ya wasomaji wake wanaopendekeza gazeti hivyo.

Lakini, uongozi huo umekubaliana na mawazo ya wachache kuruhusu umma kuanza kuchangia fedha kwa hiari ili kutoa mwanya kwa gazeti hili kuendelea kuufikia umma bure.

Sasa basi, endapo utapata kuchangia maendeleo na uhai wa Pambazuko, tafadhali tumia namba hizi kwa ajili ya mchango wako wa fedha.

Unaweza kutuma mchango wako na kuhimiza wengine kufanya hivyo kwa kuanzia shilingi 1,000 na hakuna ukomo wa kiwango cha juu; chochote kinapokelewa kwa shukrani na hakika tutatambua mchango wako. Kwetu sisi, hatuna kikubwa wala kidogo; yote ni mchango na ina thamani sava ya "asante" kutoka kwetu.

Tuma mchango wako kutoka mtandao wowote wa simu yako ya mkononi - kwenda namba hii ya Lipa kwa TIGO na utatufikia; 6214500, Pia unaweza kuchangia kupitia namba ya Mpesa: 0744 768 263

Ukitema mchango wako kupitia simu, hakikisha jina linaandaa: **Pambazuko Gazeti**. Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako - na wale wengine uliowaomba kuchagia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**.

Lipa kwa Simu

Lipa kwa kuscanner



Lipa kwa Namba

6 2 1 4 5 0 0

PAMBAZUKO GAZETI



‘Sukari anasa, weka majivu kwa chai’

Na Igo AI

ZAIDI ya wiki moja sasa, Tai kavurugwa. Hataki kuzungumza na mtu. Hataki kuonana na mtu na hataki kuambiwa lolote na yeyote.

Hata mwandishi wake hataki kuonana naye. Alimzuia kumpelekea magazeti kila siku. Akakataa kuwashwa redio ndani kwake. Akazuia runinga kuwashwa na akazima simu kwa muda wote huo.

Kijana wake wa kazi akazuiwa kusafisha chumbani kwake na kibaya zaidi, akaelekeza asipelekewe chakula mezani.

Je, nini hasa kimemsibu Tai? Kila akiulizwa na wasaidizi wake hao, hakuwa na majibu, badala yake, alionekana akitikisa kichwa kila mara, huku ‘chozi la kitu uzima,’ likimondoka.

Ijumaa iliyopita, alidamka, akabeba begi lake na kuruka kuelekea anakokujaja yeye. Hakumwambia mtu anaelekea wapi. Alionekana tu anapiga mbawa zake na kutokomea angani.

Hatimaye jana, alirejea huku sura yake ikionekana kuwa na nuru. Alikuwa na furaha kidogo. Tena akiwa amebeba kifurushi kutoka safari alikokwenda bila kuaga.

Baada ya kutua, akamuita kijana wake na kumkabidhi kifurushi na kutoa amri; “nenda ‘kicheni’ washa jiko na pasha hii nyama, nahitaji kutafuna finyango kadhaa kumkumbuka rafiki yangu aliyetangulia mbele za haki, pia usisahau kuchemsha chai ya sturungi na weka sukari nyingi.”

Tai akaingia sebuleni, akavua viatu na kushusha pumzi kidogo, huku akimuita mwandishi wake ili kupiga sogu na kumpa habari alikokuwa.

“Kwanza poleni sana, mnisamehe, nilivurugwa na taarifa za msiba wa ndugu na rafiki yangu mkubwa, Lowassa (Edward), tulishibana sana na hata alipokuwa Sauzi, nilikwenda kumsalimia,



Sukari
si mnakumbuka?”

Kumbe Tai alikuwa amechanganyikiwa kwa kifo cha Lowassa, ambaye aliwahi kuwa Waziri Mkuu wa Tanzania kwa miaka miwili na mwezi mmoja, kabla ya kuamua kujiuzulu kwa figisu za wanasiasa wenzake.

Tai akaendelea; “sasa nilitingwa kwa mawazo, sikutaka hata kwenda Karimjee kumuaga, niliamua kusubiri nikashuhudie kweli Mwamba ameingia kaburini mapema namna hii? Ndiyo maana nikaruka kwenda huko Monduli... kweli, mwenzetu amelala jumla sasa, na apumzike kwa amani ya Bwana Mungu.”

Wakati Tai na mwandishi wake wanaendelea kupiga stori, akaja kijana wake wa kazi, akamweleza; “baba hakuna umeme. Wamekata. Na sukari imeisha tangu juzi, niliogopa kukwambia.”

Ghaffa Tai akanyanyuka, akapiga kofi meza iliyokuwa mbele yake huku aking’aka; “hii nchi inakwenda wapi, hatuna umeme, hatuna maji ya uhakika, hatuna sukari, hivi kuna mdudu gani katuingilia jamani...”

Akaendelea kufoka; “Nani katuroga sisi, iweje viongozi wapo, kila mmoja anasema lwake... mwingine amezuia matumizi ya kuni tangu Januari Mosi mwaka huu, mwingine akaibuka na kusema hakutakuwa na mgawo wa umeme, yaani ni vurugu, sarakasi na mbwembwe huko serikali...”

... Yaani sasa umeme na sukari ni anasa wewe chemsha chai, weka majivu.”

Habari

Atamani Afrika itawaliwe tena

Na Scovya MANASE,
New York, Marekani

RAFIKI wa karibu, mshauri na mshirika mkubwa wa biashara wa Rais wa 45 wa Marekani, Donald Trump; anayelitwa Erik Prince, anatamani Afrika “itawaliwe tena.”

Anaitaja nchi ambayo ni sahihi kuitawala Afrika ni Marekani kwa sasa.

Prince ambaye pia ni bilionea, aliyetajirika kwa kuzaa silaha za vita kwa nchi nyingi za Afrika, anasema viongozi wengi wa bara hilo wameshindwa kuongoza nchi na watu wao.

Akizungumza Jumanne iliyopita, jijini New York, Marekani, Prince anasema viongozi wa Afrika “wameshindwa kuongoza na wanachojua, wakiwa madarakani, ni kuiba mali za umma na utajiri mwingi wa rasilimali za bara hilo kwa manufaa binafsi.”

Prince akaongeza kwamba anawatambua viongozi wengi wa bara wenye utajiri mkubwa, wakiwa wamewekeza fedha zao haramu katika visiwa na nchi tajiri zinazowakumbatia.

“Nawatambua viongozi hao wezi, kwamba wao, pamoja na umasikini wa watu wanaowaongoza, wamejaza pesa kwenye benki za nchi tajiri kwa kificho, hawana aibu hawa, ni wajinga na wanapaswa kuondolewa na nchi zao kutawaliwa na Marekani,” amesema, huku sauti yake ikisikika kuwa na ukali wenye hasira.

Alipoulizwa na mwandishi wa habari, Mark Serrano, endapo anapenda ukoloni kurejea Afrika, Prince alijibu haraka-haraka; “ndiyo napenda ukoloni urejee huko Afrika, viongozi wabovu wengi na wezi wa mali za umma. Hawawezi kuongoza.”

Prince, ambaye ni mmoja wa makomandoo wa zamani wa Jeshi la Marekani, amekuwa akipinga mapinduzi yanayofanyika katika baadhi ya nchi za



Bilionea Erik

Afrika, akieleza kuwa wanaoondolewa madarakani kijeshi, na wale wanaoingia, “ni walewale.”

Hivi sasa pamoja na biashara nyingi na nyingine anazodaiwa kufanya na Trump, pia ndiye mwanzilishi wa kampuni binafsi inayoendesha jeshi la kukodi, Blackwater.

Msimamo huo wa Prince umesikika pia katika sehemu ndogo ya video inayosambazwa na mtandao wa X (zamani Twitter), akieleza kutamani watu wa Afrika kuwa na maendeleo makubwa kuliko walivyo sasa.

Katika kuonesha namna Prince “ameshibana” zaidi na Trump, dada yake aitwaye, Betsy Devos, aliteuliwa kuwa waziri wa elimu wakati wa uongozi wa Trump.

Prince anaeleza kuwa viongozi wengi wa Afrika, wamekuwa wakipishana kwenye miji mikubwa na aghali zaidi duniani, kwenda kutalii na kufanya ununuzi wa mavazi, vito na samani zenye kulipiwa kiasi kikubwa cha fedha, huku Waafrika wengi wakilala njaa.

Anasema; “imefika wakati sasa, Marekani na dunia ikaona aibu kuacha kukumbatia viongozi wa Afrika ambao ni wezi, na dawa ni moja tu; kwenda kutawala bara hilo lenye utajiri mkubwa wa mali, lakini watu wake masikini na maendeleo ni duni mno.”

Tajiri huyo anatamani kurudi kwa ukoloni wa bendera na hata uchumi katika Afrika, ambao ulikoma kwa nchi nyingi za bara hilo kujitawala.

Malaria sasa ‘imemaliza likizo’ Z’bar

Na Mwandishi WETU

BAADA ya malaria kutokomezwa kabisa mwaka 2016, na kuipa Zanzibar hadhi ya kimataifa ya kuwa huru dhidi ya maambukizi, ugonjwa umerudi.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, wananchi 5,300 waliofika kwenye hospitali za serikali mwezi uliopita wa Januari, wamegundulika kuugua malaria.

Kati yao, watu 5,020 wametambuliwa katika hospitali na vituo vya afya vya Unguja na 230 kisiwani Pemba.

Lakini, taarifa ya kushtua zaidi ni kwamba wagonjwa 11 wamepoteza maisha kwa malaria kipindi cha Januari Mosi mpaka Januari 26, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari hivi karibuni, Ofisa Afya ya Jamii, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Zanzibar, Mwinyi Khamis, amesema kwa mwaka 2023 idadi ya watu waliogundulika na vimelea vya malaria walifikia 18,174.

Watu 17,567 kati ya hao, wamekutwa Unguja na 607 kisiwani Pemba, idadi kubwa ya waathirika wakiwa ni wanaume.

Mwinyi anayeshughulikia programu ya kutokomeza malaria Zanzibar, anasema wanaume wanaoathirika zaidi ni kundi la madereva wa pikipiki (bodaboda) wanaobeba abiria, mazingira ya kukaa maeneo yenye mbu waambukizaji malaria yakihusika.

“Mazingira ya waendesha bodaboda yamechangia sana maambukizi kutokana na mtindo wa kukaa muda mrefu kwenye, au karibu na maeneo yenye mbu wanaotoa vijidudu/vimelea vya malaria,” alisema na kuweka bayana kuwa hatari iko katika maeneo mengi ya wilaya za Zanzibar.

Kundi jingine lililoathirika zaidi na maambukizi ya malaria, anasema Mwinyi, ni mafundi ujenzi wanaofanya kazi usiku; watembezi wa sehemu za burudani nyakati za usiku na watazamaji mpira



Edward Lowassa

vijiweni usiku. Waathirika hasa ni wa umri wa miaka 15-45.

Mchango mkubwa wa kurudi upya kwa malaria, ugonjwa unaojulikana kuu kwa kasi, ni mabadiliko ya tabianchi, kuzagaa kwa maji ya mvua yanayotengeneza mazalia ya mbu wanaoeneza ugonjwa huo.

Ripoti hii inatolewa baada Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui hivi karibuni kuzindua mradi mpya wa kupambana na malaria unaofadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia shirika lake la misaada la Usaid. Dola milioni 19 zimepangwa kutumika katika mradi huo.

Mradi wa Okoa Maisha Dhibiti Malaria (OMDM) unaotekelezwa kwa ushirikiano wa asasi ya Kimarekani ya PSI, unashughulikia hatua za utambuzi wa ugonjwa, matibabu, udhibiti jumuishi wa vimelea vya malaria, ufuatiliaji na tathmini ya ugonjwa huo unaosambazwa na mbu jike aina ya anofesi.

Zanzibar ilitangazwa kuwa ‘Zero Malaria’ mwaka 2016 pale ilipokuwa imefanikiwa kushusha kiwango cha maambukizi kutoka asilimia 30 hadi asilimia 0.03 na kupata sifa kubwa kimataifa, hatua ambayo imekuwa ikielezwa kuwa moja ya sababu za kuongezeka kwa watalii.

Habari

Tumechoka mateso ya CCM – Lissu

Na Julius KISENA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimesema wananchi wa Tanzania wamechoshwa na kile kilichoita “mateso yanayoletwa na CCM” na sasa ni muda muafaka kukikataa.

Kwamba Chama Cha Mapinduzi (CCM), kinachoongoza serikali, kimekuwa chanzo cha mateso na madhila mengi yanayosababisha umasikini kwa wananchi.

Akizungumza katika Viwanja vya Furahisha, Mwanza Alhamisi iliyopita, Februari 15, Makamu wa Mwenyekiti wa Chadema, Tundu Lissu alisema CCM ndiyo chanzo cha kuwepo bei kubwa ya bidhaa muhimu, akitaja sukari kuwa miongoni.

Lissu ambaye alitumia zaidi ya nusu saa kueleza “kuchoka mateso ya CCM,” alirudia neno ‘tumechoka’ mara 22, huku akishangiliwa na umati mkubwa wa wananchi waliojitokeza kwenye hitimisho la maandamano ya amani yaliyoitishwa na chama hicho.

Alisema Watanzania wamechoshwa na maisha magumu yanayoletwa na mgawo wa umeme ambao umekosa “dawa miaka nenda rudi” na kuwa hali hiyo inasababishwa na kuwepo madarakani kwa CCM.

Makamu huyo wa mwenyekiti wa Chadema akasema wananchi wengi wanakabiliwa na njaa ya chakula kwa kuwa CCM na serikali yake, hawako makini kuhudumia wananchi, na wameshindwa kuwatumikia Watanzania kwa weledi na kufuata haki.

Lissu alisema Watanzania wamechoka kunyang’anywa mashamba na ardhi yao na viongozi wa CCM na kuwa maeneo mengi yameporwa na “wakubwa” – wakati mwingine bila kulipa fidia.

Akilalamika kuhusu uchaguzi, Lissu alisema katika uchaguzi mkuu uliofanyika miaka iliyopita, chama chake mara zote kimepokwa ushindi na CCM na viongozi wa vyombo vilivyowekwa na chama hicho



Lissu

tawala.

“Katika chaguzi zote zilizopita, Chadema imeporwa ushindi wake, wagombea wetu walishinda mara zote, lakini hawakutangazwa na watu waliowekwa na CCM, sasa tumechoka na hatutaki tena kuonewa wala kudhulumwa,” aliongeza Lissu.

Lissu alidai chama chake kilishinda viti vingi vya ubunge katika chaguzi zilizopita, kama

ilivyokuwa kwa nafasi ya urais, lakini wahusika walishindwa kuwatangaza kwa “amri kutoka juu.”

Hata hivyo, Lissu hakufafanua juu ni wapi na hakueleza majimbo aliyodai wameshinda.

Katibu wa Halmashauri ya CCM (Itikadi, Uenezi na Mafunzo), Paul Makonda, akizungumza na Pambazuko kuhusu madai ya Lissu, amesema madai ya Lissu na chama chake hayana ukweli wowote.

Makonda amesema Lissu “anaipakazia” tu CCM kwa kuwa anajua nguvu yake na namna wananchi wanavyokipenda chama hicho tawala.

Chadema imeandaa maandamano nchi nzima ikiwa na lengo la kuishinikiza serikali kuzingatia maoni na mapendekezo ya wadau mbalimbali kuhusu masuala ya uchaguzi na kulaani kuwepo maisha magumu.



Hoja Yangu

Na Rashid MTAGALUKA

Marufuku ya kope, kucha bandia imeyayuka?

NAKUMBUKA Septemba 10, 2018 aliyekuwa Spika wa Bunge la Tanzania, Job Ndugai aliwahi kupiga marufuku wabunge kuingia bungeni wakijipamba kwa kope pamoja na kucha bandia.

Uamuzi huo ulitokana na swali la Mbunge wa Viti Maalum, Fatma Toufiq juu ya athari za kiafya kwa binadamu kwenye matumizi ya mapambo hayo bandia pamoja na kujichubua ngozi.

Ndugai ambaye 'aliachia ngazi' kwenye nafasi hiyo, alisema marufuku hiyo ingewahusu pia wageni wote watakaokitembelea chombo hicho kilichoko jijini Dodoma, bila kufafanua uhusiano wa wageni hao na marufuku hiyo.

Hata hivyo, licha ya naibu waziri wa afya wa wakati huo, Dkt Faustine Ngugulile kuueleza mhimili huo wa dola kuwa, matumizi ya urembo huo bandia yana athari kubwa kwa binadamu na kuitaka jamii kuepukana nayo, haikuonekana kutiliwa nguvu!

Serikali ya Tanzania ya wakati huo haikulitilia maanani na mpaka sasa hatuoni jambo hilo likitiliwa mkazo pamoja na kwamba, athari za matumizi ya urembo huu inaelezwa ni kubwa kwa kadiri siku zinavyokwenda.

Kwa mfano, Dkt Ndugulile aliwahi kueleza kuwa, kwa mwaka mmoja, takriban wagonjwa 700 hupokelewa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili peke yake wakiwa na matatizo ya ngozi yanayotokana na kujichubua.

Tangu mwaka 2018 sijawahi kufuatilia iwapo agizo na marufuku ya Ndugai inatekelezwa bungeni mpaka sasa au alipojiuzulu nafasi hiyo na utekelezaji wa agizo hilo nao 'ukajiuzulu.'Sijui!

Hata hivyo, nina uhakika ni kukosekana uthabiti kwa mamlaka zenye dhamana ya kulinda afya za wananchi wake katika kuhakikisha bidhaa zilizopigwa marufuku haziingii nchini.



Kope bandia

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Dkt. Athuman Ngenya 'akitema cheche' kuhusu marufuku ya bidhaa hizi, alisema; "kope, kucha, rangi vimekatazwa, na nichukue nafasi hii kutoa tahadhari kwa wafanyabiashara wa bidhaa hizi kuhakikisha wanaviondoa sokoni, vinginevyo tukifika tutawachukulia hatua za kinidhamu."

Baada ya kumsikiliza kwa makini mwanasayansi huyo mbobezi hapa nchini aliyeteuliwa kuisimamia TBS, nikajiuliza maswali mengi yaliyokosa majibu haraka. Kwanza, ipo sheria mahususi iliyotungwa na Bunge kupiga marufuku ingizwaji wa kope, kucha na rangi zake kama ilivyo kwa dawa za kulevya au kukutwa na nyara za serikali?

Kama sheria hiyo ipo, kwanini mamlaka zinatumia muda mrefu kuwabembeleza wanaoingiza pamoja na watumiaji wa bidhaa hizo zinazoeleza kuwa ni hatari kwa afya ya binadamu?

Mbona hatuoni mamlaka zikijishughulisha kuviamrisha vyombo vyake vilivyopewa dhamana ya kusimamia na kuhakikisha sheria zilizotungwa na Bunge zinafuatwa, vinachukua hatua dhidi ya wavunja sheria hawa?

•**Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari anapatikana kwa simu namba 0784 438546 au barua-pepe:mtagaluka@gmail.com**

Habari

China kufufua Tazara kwa triloni 2.6/-

Na Peter ANDREA

CHINA inapanga kutumia dola za Marekani bilioni moja kukarabati njia kuu ya reli inayounganisha eneo la ukanda wa shaba wa Zambia na Bandari ya Dar es Salaam, Tanzania.

Balozi wa China nchini Zambia, Du Xiaohui amekabidhi pendekezo la kukarabati reli ya hiyo – maarufu Tazara, kwa Waziri wa Uchukuzi wa Zambia, Frank Tayali, na kueleza kuwa uwekezaji huo wa dola za Marekani bilioni moja, sawa na Sh. triloni 2.6, utafanywa kupitia ushirikiano wa sekta ya umma na binafsi (PPP), hivi karibuni.

Du amesema China itashirikiana na “ndugu zake wa Zambia na Tanzania” ili kuimarisha ushirikiano na kuzinufaisha nchi hizo tatu, huku wananchi wakipata huduma bora na kisasa zaidi.

Pambazuko linazo taarifa kuwa timu ya wataalamu wa usafiri wa reli kutoka China, wamekamilisha uchambuzi yakinifu wa kubaini endapo reli hiyo bado inaweza kuwa chachu ya kukua kwa uchumi kwa nchi na wahusika wengine.

Timu hiyo ambayo ilifaya kazi hiyo kuanzia Desemba, mwaka jana, imekamilisha ukaguzi wa kibiashara na kiufundi wa Mamlaka ya Reli ya Tanzania-Zambia, waendeshaji wa Tazara, na kwamba iliwasilisha ripoti yake Jumatano iliyopita.

Tayali amesema Zambia pamoja na mshirika wake, Tanzania, zinapokea mpango huo kwa furaha kubwa, huku nchi hizo zikiamini “makubwa yanakwenda kutendeka” ili kurejesha heshima ya reli hiyo.

Marais wa Tanzania na Zambia walipotembelea China mwaka 2022 na 2023 mtawalia, Rais Xi Jinping wa China aliahidi kuunga mkono uboreshaji wa reli hiyo ambayo awali ilijengwa miaka ya 1970 na kufadhiliwa na Serikali ya China,



Treni ya TAZARA

chini ya kiongozi wake, Mao Zedong, ukiwa ni mradi wa msaada.

Xi alisema Reli ya Tazara imekuwa “ishara ya urafiki kati ya China na Afrika” na kwamba sasa itafanyiwa ukarabati mkubwa ili kuendelea kuenzi uhusiano wake na Afrika.

Mwaka jana, China ilitewa shirika la ujenzi na uhandisi la nchi hiyo (CCECC), kampuni tanzu ya Shirika la Ujenzi wa Reli la China, kufanya mazungumzo ya makubaliano ya kukarabati na kuendesha njia ya Reli ya Tazara kwa ubia.

CCECC ilitewa timu ya watu 11 ikiongozwa na Peng Danyang, Mkurugenzi Mkuu wa Reli ya Ethiopia-Djibouti, kufanya ukaguzi kutoka Dar es Salaam hadi Kapiri Mposhi nchini Zambia kwa lengo la kutathmini namna ya kuendesha reli hiyo na kuchunguza mfumo wa biashara wa Tazara.

Reli ya Ethiopia-Djibouti ambayo ni ya kisasa zaidi, inaendesha kwa ubia na China.

China ina lengo la kutumia njia ya Reli ya Tazara kusafirisha bidhaa za madini kutoka Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kuelekea China.

Mtanzania mbaroni India kwa cocaine

Na Tryruckia MFINANGA

SIFA ya Tanzania kuwa chaka la dawa za kulevya zinaendelea kushika mizizi dunaiani kila uchao kwa taarifa za kutumika “kutengenezwa ama kuwa chochoro” la kuzipitisha.

Hilo limethibitika tena jana wakati Mtanzania aliyetajwa kwa jina la Hassan Mwinyi Mchonga, miaka 36, kukamatwa akiwa na gramu 153 za dawa za kulevya aina ya cocaine, zinazoeleza na Polisi wa India kuwa na thamani inayokaribia shilingi milioni 100 za Tanzania.

Kikosi cha Kupambana na Dawa za Kulevya India (ANC), katika Mji wa Pune, kimesema Mtanzania huyo alikamatwa juzi, baada ya wale walioitwa wasamaria wema kutilia shaka mienendo ya maisha yake na kutoa taarifa.

Polisi wa India wanaeleza kuwa Hassan alikutwa na “mzigo” huo katika nyumba ya ghorofa alimopanga katika eneo la Undri.

Taarifa zilizoifikia Pambazuko juzi na maendeleo yake kuthibitishwa jana, zinaeleza kuwa Mtanzania huyo aliingia India akiwa na pasi ya kusafiria yenye hadhi ya kufanya biashara.

Inspekta wa polisi eneo la Pune, anayehusika na ANC, Anita Hivarkar amesema kuwa mtuhumiwa huyo aliingia India mwanzoni mwa mwaka huu, akiwaeleza maofisa wa Uhamiaji kuwa ni mfanyabiashara wa nguo.

Wakati anakamatwa, visa ya kuwepo India ilikuwa bado haijaisha.

Polisi wanasema Mtanzania huyo atafikishwa mahakamani leo - Jumatatu kujibu tuhuma dhidi yake za kujihusisha na biashara ya dawa za kulevya.

“Bado tuko naye na tunamuhaji alivyoingia na dawa hizo kwenye ardhi ya India, lakini pia tunataka kufahamu anashirikiana na watu gani, kutoka wapi na aeleze wapi zinatengenezwa



Cocaine

dawa hizo, hapo sasa tutamfikisha mahakamani. Huenda hilo likafanyika kesho,” anasema Anita.

Tanzania imekuwa ikigonga vichwa vingi vya vyombo vya habari duniani, hasa baada ya shehena kubwa kukamatwa hivi karibuni katika maeneo ya Kigamboni, Dar es Salaam, na Iringa.

Hivi karibuni, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Tanzania(DCEA) ilifanikiwa kukamata jumla ya kilo 3,182 za dawa za kulevya aina ya heroin na methamphetamine katika operesheni maalum iliyofanyika kwenye mikoa hiyo.

Katika operesheni hiyo ambayo ilifanyika kwa siku 18 tu; kuanzia Desemba 5 hadi 23,mwaka jana -2023, watu saba walikamatwa.

Akizungumza na waandishi wa habari Desemba 27,2023 Dar es Salaam, Kamishna Jenerali wa DCEA, Aretas Lyimo alisema kiasi hicho cha dawa za kulevya kinajumuisha kilo 2,180.29 za dawa aina ya methamphetamine na kilo 1001.71 aina ya heroin.

Lyimo alisema kukamatwa kwa shehena hiyo ni historia, kwani Tanzania hajawahi kuwakamata wahusika wenye kiasi kikubwa cha dawa hizo haramu.

Miji mikubwa ya Dar es Salaam, Zazibar, Arusha, Mwanza na Tanga ndiyo inaelezwa kuwa kinara wa matumizi ya dawa hizo haramu.

Tafakuri

Bagonza amlilia Lowassa, aweka maono

JUZI, Jumamosi ya Februari 17, tumemzika Edward Ngoyai Lowassa nyumbani kwao Monduli, Arusha.

Miaka 40 iliyopita tulimzika Edward Moringe Sokoine katika eneo hilohilo la Monduli.

Tulivyomzika Edward yule, ndivyo tumemzika Edward huyu. Jina “Edward” lina maana kubwa katika eneo hilo hata kama sijui.

Yalikuwa ni mazishi yenye hadhi. Usingejua kama ni ya waziri mkuu mstaafu. Waziri mkuu yeyote aliye madarakani bado yangemfaa. Yaliandaliwa chini ya uenyekiti wa waziri mkuu aliyeko madarakani, Kassim Majaliwa. Kazi nzuri.

Miongoni wa waliohudhuria mazishi ni huzuni, fahari, furaha, aibu na fundisho.

Nilitafakuri yafuatayo katika kumuenzi Edward Lowassa;

Kwamba Edward aliondoka Monduli mara ya mwisho akiwa amesimama. Amerudi amelala. Kulala na kusimama; yote mawili yana nguvu na hadhi sawa. Tuwe wanyenyekevu.

Kwamba Edward ameliunganisha taifa letu japo kwa siku moja. Wote tulikaa kwa adabu na utulivu na kusahau kwa muda tofauti zetu. Wote tulitumia “washroom” zile zile bila kubaguana. Kumbe inawezekana?

Kwamba mishangao yangu; kutowaona niliodhani wangekuwepo. Kuwaona niliodhani hawawezi kuwapo. Kupopoa historia ya Edward iliyobeba haiba yake ya “uamuzi mgumu.”

Kwamba ilipigwa mizinga: Mimi nilihesabu 16, jirani yangu akahesabu 17. Jirani wa upande wa pili akasema litakiwa 21.

Timu ya wana itifaki wa serikali na jeshi wakatahadhalisha wenye mimba; wakasahau tuko wajinga wengi tusiojua mizinga 16/17 au 21 ina maana gani? Akifa mwingine mtueleze tafadhali!

Kwamba Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe “aliiiba onyesho”



Edward Lowassa

msibani.

Alipata fursa kusalimika kama mwana familia. Akainadi Chadema. Akaboresha historia ya Edward. Mama akaikamilisha. Siku yenye huzuni ikaisha vizuri. Tukasikia makofi msibani.

Kwamba tulipomzika Edward Sokoine, tulizika darasa la uongozi. Kwa kumzika Edward Lowassa, twaweza kuwa tumezika maabara ya uongozi.

Mmoja aliamini katika ufukara mtakatifu. Mwingine katika utajiri-uzalendo. Tusihemuke, tutafakuri.

Upo uhusiano wa matumbo yao na dhamana waliyopewa; matumbo yao yanapanuka wakati dhamana na taasisi zao zinakonda. Hawana kiu ya haki tena.

Kwamba Monduli ilikuwa ndogo siku ya mazishi. Msiba ukahamia kwenye ng’ombe. Watu walizoea kula nyama alipokuwa hai. Wamekula zaidi alipokufa. Tupo ambao hatukusikia njaa pamoja na kutokula.

Kwamba Kwaresima ya 2024 tutaikumbuka kwa kushinda njaa tukikuzika. Fredy Lowassa umuenzi babako daima kwa kuwapa watu nyama walizozioea alipokuwa hai.

Kawamba nilitamani aliyemteua Lowassa kuwa waziri mkuu atusalimie. Haikutokea.

Ukisikia msiba, hiyo ndiyo maana yake. Ukipenda, mnyime mengine, lakini ni muungwana. Alihudhuria.

Makala haya ya tafakuri, yameandikwa na Askofu Dkt. Benson Bagonza wa KKKT, Karagwe.

Nenda salama Lowassa

Lala Salama 'Mwamba' Kwaheri Lowassa, tutaonana baadaye



Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan akiweka shada la maua kwenye kaburi la Lowassa.

Kutoka kushoto: Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, mfanyabiashara maarufu, Rostam Aziz, Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe na Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe wakiweka shada la maua kwenye kaburi la Edward Lowassa, waziri mkuu mstaafu aliyefariki dunia Februari 10, na kuzikwa kijijini kwake Ngarash, Monduli, Arusha juzi – Jumamosi, Februari 17, 2024. Wote hawa wametajwa kuwa marafiki wa karibu zaidi wa Lowassa.



Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Tulia Ackson akiweka shada la maua kwenye kaburi la Lowassa. (Picha zote na Ikulu).

Mhariri Mkuu wa Pambazuko, wahariri, waandishi na watendaji wote wa gazeti hili wanawapa pole familia, ndugu, jamaa na Watanzania wote kwa kuondokewa na Edward Lowassa na kumtakia pumziko jema la milele huko alikopokelewa.

Tangazo



Tangaza na **Pambazuko**

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi

Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua huduma na biashara yako.

Kwa bei nafuu sana

0744 768 263 au

Barua- Pepe; info@pambazuko.tz

Marekani yajitokeza kulaani Rwanda

Na Mwandishi MAALUM

MAREKANI imetangaza waziwazi kwamba inalaani Rwanda kwa kuunga mkono kundi la waasi la M23 linaloendelea kutishia amani Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Nchi hiyo inayotajwa kuwa tajiri zaidi duniani, imeeleza kwamba inatambua kuwepo kwa kila dalili Rwanda kusaidia waasi hao kwa silaha na fedha ili kuendelea “kuvuruga amani na maendeleo ya DRC.”

Katika taarifa yake iliyofikishwa kwenye vyombo vya habari juzi na Pambazuko kupata nakala yake, Marekani inaitaka Rwanda kuacha mara moja “kusaidia mipango ya M23.”

Marekani inaeleza kuwa Rwanda kuunga mkono waasi hao, ni kuruhusu mauaji kuendelea, huku kukisababisha kuwepo kwa wakimbizi wengi bila sababu za msingi.

Kundi la waasi la M23 limeweka kambi zake maeneo ya mashariki mwa DRC na kusababisha idadi kubwa ya Wacongo kuyakimbia maeneo yao ili kulinda uhai wao.

Inadaiwa kuwa misaada ya Rwanda kwa kundi hilo la waasi, yanalenga kupoka mali za DRC, hasa madini yanayopatikana nchini humo kwa manufaa binafsi ya nchi hiyo inayoongozwa na Rais Paul Kagame.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani katika taarifa yake imekosoa vikali hasia zinazoendelea katika eneo hilo la mashariki na kutamka kwamba ni wakati muafaka sasa M23 kuacha machafuko.

Marekani pia imeitaka Rwanda kuondoa wanajeshi wake walioko katika kikosi cha kulinda amani DRC na kuhakikisha mifumo yake ya makombora ya ardhini na angani, yanaondolewa haraka.

Kwamba kuondolewa kwa majeshi hayo kutaleta utulivu hata kwa makundi mengine ya wanajeshi wanaolinda amani



Rais Tshisekedi

na maendeleo ya DRC.

“ Kuendelea kuwepo kwa mifumo ya makombora ya kunatishia maisha ya raia wa DRC na kwamba hata walinda amani wanashindwa kuwa na uhakika wa uhai wao,” imeeleza taarifa hiyo.

Pia iliwataka waasi kuondoka katika maeneo wanayokalia ambayo yako karibu na maeneo mawili ya mijini kwenye Jimbo la Kivu, nchini DRC.

Wachambuzi wa masuala ya vita na amani kutoka DRC wanadai kuwa Marekani imetoa taarifa hiyo kwa lengo la kushinikiza Rwanda kuchukua hatua haraka kuondoa majeshi yake na kuacha kusaidia waasi hao wa M23.

Pamoja na kwamba Rwanda hadi sasa haijajibu chochote kufuatia taarifa hiyo ya Marekani, lakini mara zote imekuwa ikikanusha kuwasaidia waasi hao wa M23, wala wengine wowote walioko DRC ama maeneo mengine.

Rais Kagame amekuwa akinukuriwa kueleza kwamba kinachofanywa na mataifa mengi makubwa kwa kutuhumu nchi yake kusaidia waasi, ni hisia tu zisizokuwa na “kichwa wala miguu.”

Rais wa DRC, Felix Tshisekedi, kama inavyodai Marekani, amekuwa akiishutumu Rwanda kwa kuivuruga amani ya nchi yake kwa kusaidia waasi wa M23.

Kazakhstan

Walawiti, wabakaji kukatwa uume

Na Mwandishi MAALUM

SERIKALI ya Kazakhstan inapanga kuanza kutoa adhabu ya kukatwa uume kwa watu watakaopatikana na hatia ya kubaka na kulawiti watoto.

Mchakato wa kupitishwa kwa sheria hiyo umepamba moto ndani ya bunge la nchi hiyo, huku wanaharakati wa haki za watoto wakivalia njuga kuharakishwa kwake.

Ikiwa hatua hii itapitishwa na kusainiwa na rais wa nchi hiyo kuwa sheria, itafuta adhabu ya zamani ya kuwahasi waliokuwa wakithibitika kufanya kosa la kubaka, kulawiti na kudhalilisha watoto kwa njia za kingono.

Awali, wenye hatia, walikuwa wakihasiwa kwa njia ya kitabibu – katika hospitali za serikali, adhabu ambayo inadaiwa kuwa “haitoi vitisho kwa wengine kufanya kosa hilo au waliohasiwa kurudia kosa.”

Wabunge wengi wanaeleza kuwa utaratibu wa wanaume wenye makosa ya kulawiti kuhasiwa kwa kemikali, kumeshidwa kuwazuia watu wenye tamaa na ngono kwa watoto.

Elnur Beisenbaev, mbunge na Katibu Mtendaji wa Chama cha Amanat, amesema serikali inapaswa kuwa mstari wa mbele kuhakikisha kuwa wanaothibitika kufanya makosa ya ngono dhidi ya watoto “wanakatwa uume haraka.”

Mtendaji huyo wa chama tawala, anasema kuwa pamoja na adhabu ya kuhasiwa inaogofya, bado matukio ya watoto kubakwa na kulawitiwa yanafanyika kwa kasi. Hayaonekani kupungua, hivyo adhabu stahiki ni kukatwa uume.

“Ikiwa shambulio kingono kwa watoto ni la kikatili sana, ninaamini kukatwa uume ndiyo adhabu inayostahili ili kutoa onyo kwa wengine wenye tabia ama matamano ya namna hiyo,” anasema mwanaharakati wa haki za watoto nchini humo, Yuzleb Ghazer.



Vifaa vya upasuaji hospitalini

Anasema kuwa adhabu ya kuhasiwa kwa wanaume wenye makosa hayo, inaonekana kuwa ndogo, ndiyo maana hata wengine bado wanafanya makosa hayohayo na kila mara.

Inaelezwa kuwa kuhasiwa kitabibu kwa wanaume wengi, hakuondoi hamu ya kufanya mapenzi kwa kiasi kikubwa kama ambavyo iliaminika awali wakati wa kupitishwa kwa adhabu hiyo.

Alizungumzia kisa kimoja alichokielezea kuwa kibaya zaidi, ambacho kimegonga vichwa vya habari nchini humo karibuni, mwanaharakati huyo anasema ameshangazwa na mahakama kuamua kifungo cha miaka 20 kwa baba kumbaka binti yake kwa miaka miwili mfululizo.

“Huu ni upuuzi. Wahalifu kama yeye wanapaswa kukatwa uume na kufungwa jela maisha, kuliko kuasiwa wala kupewa adhabu nyingine yoyote,” ameongeza mwanaharakati huyo.

Mwanaharakati mwingine wa haki za binadamu, Dina Tansari anasema baadhi ya vijana wenye umri mdogo wanapopatikana na hatia ya kulawiti ama kubaka, wamekuwa wakipewa adhabu ya kuhasiwa, lakini bado, kadri wanavyokuwa, “wanaendelea kuwa hatari.”

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani wa Kazakhstan, Igor Lepikha alisema kuhasiwa kwa upasuaji kulikuwa na ‘utata,’ hivyo adhabu mpya, inayopendekezwa inaweza kuwa suluhisho na kuokoa watoto wasiokuwa na hatia.

Rugambwa akabidhiwa kanisa Italia

Na Benedict Msoffe,
Roma

KARDINALI Protase Rugambwa, Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Tabora, Tanzania, jana alikabidhiwa la “Santa Maria in Montesanto”, lililoko kwenye Barabara la Babuino, namba 198, huko Roma, Italia.

Kukabidhiwa kwa kanisa hilo, sasa Kardinali Rugambwa anakuwa sehemu ya Wakleri wa Roma, wanaounda Baraza la Makardinali lenye jukumu la kumsaidia kiongozi wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis.

Makardinali kimsingi ndio washauri wakuu wa Papa ili kukoleza majukumu yake ya kuhamasisha toba, haki, amani na maridhiano; kwa kukuza na kudumisha utu na heshima ya binadamu, ili watu waweze kuishi katika mazingira bora zaidi.

Papa Francisko Aprili 13, 2023 alimteua Protase Rugambwa kuwa askofu mkuu mwandamizi mwenye haki ya kirithi Jimbo Kuu la Tabora, Tanzania na Julai 9, mwaka huohuo akamteua kuwa kardinali wa tatu kutoka Tanzania na kusimikwa rasmi Septemba 30, 2023.

“Sasa Kardinali Rugambwa anakwenda kunitwaa kiti chake cha heshima katika Kanisa (Basilika) la Bikira Maria la Mlima Mtakatifu (La Basilica di Santa Maria in Montesanto) huko Roma, Italia,” mmoja wa wanafunzi wa theolojia anayetoka Tanzania ameliambia Pambazuko.

Katika kanisa hilo liliadhimishwa Ibada maalum ya misa ikiingozwa na Kardinali Protase Rugambwa.

Katika misa hiyo lilifanyika pia tendo la Kardinali Rugambwa kutwaa rasmi mamlaka yake juu ya kanisa lake hilo la “Kikardinali”.

Kwa asili, makardinali wanateuliwa kumsaidia Papa, ambaye pia hutambulika kuwa ni Askofu wa Roma katika shughuli



*Kanisa alilopewa
Kardinali Rugambwa*

za kichungaji jimboni.

Inaelezwa kuwa makardinali hupewa kusimamia makanisa fulani katika jimbo hilo na hawalazimiki kukaa hapo kwani pia wanapaswa kuwepo kwenye maeneo yao.

Hata hivyo, kwa kuwa nafasi yao inadai kuwepo na ukaribu wa pekee na makazi ya Papa, makardinali wengi hulazimika kuhudumu katika makanisa hayo mara kwa mara.

“Ni muhimu sana makardinali wanaopewa makanisa hapa Italia kuwa hapa, lakini, ikumbukwe kuwa, mamlaka yao katika makanisa hayo si mamlaka halisi bali ni “ishara tu” ya umoja wao na Papa,” anaongeza mwanazuoni uyo wa theolojia.

Utendaji na uungalizi wa karibu, na ule wa kila siku wa makanisa hayo hubaki chini ya mamlaka anayoiteua yeye insaidie katika kutekeleza hayo.

Kwa mantiki hiyo, Mwadhama Kardinali Rugambwa, kiutendaji anabaki kuwa Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Tabora nchini Tanzania.

Kuutwaa kwake usimamizi wa Basilika la Santa Maria in Montesanto, Roma nchini Italia, kunakamilisha tu yale matendo yenye ishara ya umoja wa Kardinali na Papa.

Makala

Tunalea janga mabasi kubeba mafuta

Na Abdulrasul ELHAJI

TUKIO la ajali ya moto lililotokea Agosti 10, 2019 lililotokana na mlipuko wa roli la mafuta maeneo ya Msamvu, Morogoro, limenikumbusha hatari inayoweza kutokea wakati wowote kwenye magari ya abiria yanayofanya safari zake kati ya mijini na vijijini.

Katika tukio hilo ambalo sasa lina miaka zaidi ya minne, liliacha majonzi na simanzi, siyo tu kwa wakazi wa Morogoro, lakini pia na nchi nzima kwa ujumla kufuatia watu zaidi ya 100 kuripotiwa kupoteza maisha na wengi kadhaa kujeruhiwa.

Ingawa mazingira na chanzo cha ajali ile haviwezi kulinganishwa na haya ninayotahadharisha hapa, lakini madhara yatakayotokana na mlipuko wa mafuta kwenye magari ya abiria kusipochukuliwa tahadhari haraka, yatajurejesha kwenye tukio la Msamvu.

Ni wazi sasa kwamba kufuatia tukio lile, nilitarajia machungu ya ndugu zetu hao yanatosha kuwa funzo kubwa kwa kila Mtanzania na kuweza kuchukua hatua na kutekeleza wajibu kwa kila hatua pale inapobidi.

Hata hivyo, inaonesha walio wengi wakiwemo wasimamizi wa sheria zetu, pamoja na vyombo vingine vya dola, hawawajibiki ipasavyo au wanawajibika, lakini kuna mahala wanapigwa chenga na wafanyabiashara ya usafirishaji abiria.

Changamoto ya ukosefu wa vituo vya mafuta kwenye maeneo mbalimbali ya vijiji vyetu hapa nchini, inaweza kugeuka dhahma na kuweka rehani maisha ya Watanzania wengine wanaotumia mabasi, ambayo yanabeba pia madumu ya mafuta.

Wamiliki wa vyombo hivi vya usafiri wa abiria wanaweza wasiwe na taarifa, lakini madereva na makondakta wa magari yao, yanatumika kubeba madumu ya petroli kwenye basi moja na abiria.

Hatusemi na wala hatumaanishi



Basi limewaka moto baada ya mafuta ya petroli yaliyobebwa ndani ya madumu kulipuka

kwamba, wakazi wa vijijini hawapaswi kupatiwa huduma ya kupelekewa nishati hii muhimu kwa maendeleo yao hapana, lakini kama tutaendelea na utaratibu huu wa sasa pasi na wenye mamlaka ya kusimamia sheria kuchukua hatua, ipo siku tutakuja kuomboleza!

‘Utamaduni’ huo umeshuhudiwa kwenye mabasi ya abiria yakiwa na shehena ya mafuta kwenye wilaya za Masasi, Tandaimba, Newala mkoani Mtwara, Nachingwea, Kilwa, Liwale, Ruangwa mkoani Lindi na magari yote yanayokwenda Morogoro vijijini, Kilosa, Ifakara na Mvomero mkoani Morogoro.

Sijui ugumu uko wapi kwa wafanyabiashara wa bidhaa hii kuagiza kwa kutumia magari maalumu yenye matenki ya kubebea mafuta na hivyo kufanya bidhaa hiyo kuwa salama zaidi kwa upande mmoja na wao wenyewe kwa ujumla wake.

Sisemi wafanyabiashara wasiuze mafuta huko vijijini kwa uwazi kabisa, hapana, maana natambua umuhimu wa huduma hii inavyosaidia kusukumama mbele shughuli za maendeleo, lakini tukitafuta njia sahihi ya kufikisha mafuta hayo kwenye maeneo yetu, itatusaidia zaidi kuliko kuweka kwenye magari yanayobeba vyakula na abiria pamoja.

Mwandishi ni mchambuzi masuala ya jamii-kazi xa sanaa na mhifadhi wa utamaduni wa Afrika, anapatikana kwa simu namba; 0710103273

Kipchoge, Kiptum hawakutani tena

Na Geoffrey ANENE

VITA vya ubabe vilivyokuwa vikisubiriwa kwa hamu kubwa kwenye mbio za kilomita 42 kati ya wakenya wawili wababe wa 'kufukuza upepo,' sasa havitakuwepo.

Vimekatizwa na kifo cha mmoja wao, Kelvin Kiptum.

Kiptum, pamoja na mwanariadha anayetamba kwa sasa duniani, Eliud Kipchoge walitarajiwa kuchuana vikali baadaye mwaka huko katika michuano ya Olimpiki iliyopangwa kufanyika Paris, Ufaransa.

Kiptum alifariki Jumapili iliyopita baada ya kupata ajali ya gari.

Kipchoge, 39, na Kiptum, 24, walitiwa katika kikosi cha Kenya cha marathon kitakachoshiriki Michezo ya Olimpiki kuanzia mwezi Julai hadi Agosti, mwaka huu.

Wakenya hao wawili hawakuwahi kkuutana katika mashindano mengine yoyote na mashabiki walikuwa wakisubiri kwa hamu kuona nani ataibuka mbabe kato ya wawili hao, wanaobeba sifa kubwa za kuwa mahiri katika riadha.

Kiptum alikuwa binadamu wa kwanza kukamilisha mbio rasmi za kilomita 42 chini ya saa mbili na dakika moja baada ya kushinda Chicago Marathon kwa saa 2:00:35 mwezi Oktoba mwaka jana, 2023.

Alifuta rekodi ya Kipchoge ya 2:01:09 ambayo ilikuwa imewekwa Septemba,



Kipchonge



Kiptum

2022 jijini Berlin, Ujerumani.

Kiptum alikuwa tayari ameanza kubatizwa kuwa ndiye mfalme mpya wa mbio za kilomita 42 baada ya kutawala mbio za Valencia Marathon nchini Uhispania kwa 2:01:53 mnamo Desemba 2022; London Marathon kwa 2:01:25 (Aprili 2023) na Chicago Marathon (Oktoba 2023).

Kifo chake kimetokea miezi michache baada ya kutawazwa kuwa ni Mwanariadha Bora Duniani wa mbio ndefu mwaka 2023 mwezi Desemba.

Rekodi yake ya dunia ya 2:00:35 pia ilirasimishwa siku chache zilizopita.

Kiptum ameaga dunia pamoja na kocha wake Gervais Hazimana kutoka Rwanda.

Inaelezwa kuwa Kiptui alikuwa anajiandaa kufungua msimu kwa kutimka kwenye mbio za Rotterdam Marathon nchini Uholanzi hapo Aprili 14, alikenga kuimarisha rekodi yake ya dunia.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi wa Marakwet, Peter Mulinge, mwanariadha Kiptum alikuwa anaendesha gari aina ya Toyota Premio, akiwa na Garvais na mwanamke aliyetambuliwa kama Sharon Kosgey, wakielekea nyumbani kutoka maeneo ya Eldoret wakati gari lake lilipoacha barabara na kugonga mti katika eneo la Kaptagat.

Sharon alinusurika, lakini akiwa na majeraha makubwa. Alikimbizwa katika Hospitali ya Racecourse, huku miili ya Kiptum na Garvais ikapelekwa mochari ya hospitali hiyo.

Huu ndio upinde wa mvua



Upinde wa mvua uliponaswa jana – Jumapili saa 6:02 mchana kutoka eneo la Vwawa, Mbozi, Mbeya. Ni nadra sana hali hii kutokea. (Picha na Godfrey Mwakitwange).

GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa msunguko – kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.

